EAST AFRICAN CRUDE OIL PIPELINE







# MUHTASARI WA TATHMINI YA ATHARI ZA KIMAZINGIRA NA KIJAMII TANZANIA



# UTANGULIZI

Andiko hili linaelezea kuhusu mradi wa Bomba la Mafuta Ghafi la Afrika Mashariki (EACOP) na Tathmini ya Athari za Kimazingira na Kijamii (ESIA) iliyofanywa na mradi.

Andiko linafafanua aina za athari zinazoweza kutokea kwa jamii husika pamoja na mazingira. Pia linatoa ufafanuzi wa nini kitafanyika katika kutatua au kuzikabili athari hizo.



Bomba hili litasafirisha mafuta ghafi kutoka wilaya ya Hoima nchini Uganda mpaka kituo cha kuhifadhia mafuta kilichopo jiji la Tanga, karibu na kituo cha kupakia na kusafirisha mafuta. Mradi huu nchini Tanzania unajumuisha:

- Bomba lenye urefu wa kilometa 1147, na kipenyo cha inchi 24 litakalofukiwa ardhini kuanzia mpaka wa Uganda na Tanzania hadi rasi ya Chongoleani iliyopo kaskazini mwa Tanga.
- Miundombinu ya juu ya ardhi inajumuisha: vituo vinne (4) vya pampu zinazo sukuma mafuta ili yaweze kupita kwenye bomba kutoka magharibi mpaka mashariki, vituo viwili (2) vya kupunguza kasi ya msukumo wa mafuta katika sehemu ya bomba la mafuta linalokatisha sehemu ya mwinuko wa ardhi kuelekea pwani ili kupunguza kasi ya msukumo wa mafuta kabla ya kufika katika matanki ya kuhifadhia mafuta, valvu 60 katika vituo muhimu ambapo mtiririko wa mafuta unaweza kupunguzwa au kuzuiliwa, vituo 21 vya umeme vya kuongeza nguvu ya umeme, tanki la kuhifadhi mafuta karibu na ghuba ya Tanga, gati yenye urefu wa kilometa 1.9 ili kusaidia bomba lililopo juu ya ardhi kusafirisha mafuta kutoka katika tenki la kuhifadhi mafuta mpaka kwenye gati ambapo mafuta yatapakiwa katika meli kubwa.
- Kambi 12 pamoja na maeneo ambayo yatatumika kuhifadhi mabomba, nyumba za wafanyakazi wakati wa ujenzi, na vituo vya kufunika mabomba ili yaweze kutunza joto.












# MCHAKATO WA TATHMINI YA ATHARI ZA KIMAZINGIRA NA KIJAMII

Tathmini ya athari za Kimazingira na Kijamii (ESIA) imefanyika kwa kuzingatia sheria na taratibu za Serikali ya Tanzania. Athari chanya na hasi kwenye uchumi, watu na mazingira zimeelezwa na kufanyiwa tathmini kwa kupitia nyaraka mbalimbali na tafiti za kimazingira na kijamii. Zaidi ya hapo, kumekuwepo na ushirikishwaji wa jamii hasa za waguswa wa mradi ili kupata taarifa mbalimbali, uelewa wa jamii juu ya athari zinazoweza kutokana na mradi huu na hatua zinazoweza kuchukuliwa ili kupunguza athari hizo. Haya yote yamejumuishwa katika Tathmini ya Athari za Kimazingira na Kijamii.

Tathmini hii ilifanyika kwa zaidi ya miaka miwili (2017-2018) na ilipitia hatua zifuatazo:

01 Utambuzi wa awali wa athari zinazoweza kutokea kwa kupitia machapisho au nyaraka mbalimbali.

02 Utambuzi wa athari kubwa zinazoweza kutokea ili kufanya tathmini ya kina.

03 Tafiti za awali ili kukusanya taarifa zitakazowezesha kutoa uelewa mpana juu ya hali ya kimazingira na kijamii.

04 Utambuzi wa athari za mradi.

05 Uchukuaji wa hatua mbalimbali zitakazo wezesha kupunguza athari.

06 Kukusanya na kuzinakili kwa pamoja hatua za kudhibiti athari za kimazingira na kijamii kwenye mpango wa utekelezaji.

07 Utambuzi wa hatua za ufuatiliaji zinazohitajika, kuziingiza katika mpango wa ufuatiliaji wa masuala ya kimazingira na kijamii.

Kabla ya ujenzi wa bomba la mafuta, mradi utaandaa mikakati na mipango mbalimabli ili kusaidia utekelezaji wa masuala ya mazingira na jamii. Mradi utahikikisha mikakati na mipango hiyo inatekelezwa kwa mujibu wa sheria, wakati wote wa ujenzi na uendeshaji wa mradi.

Tathmini hii ilishirikisha Shirika la Taifa la Mafuta la Uganda (Uganda National Oil Company), Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania (Tanzania Petroleum Development Corporation), waendelezaji na waendeshaji wa Bomba la Mafuta Ghafi Afrika Mashariki (Total E&P Uganda, Tullow Uganda Operations Pty Ltd , CNOOC Uganda Limited) na Total East Africa Midstream BV.

# MUHTASARI WA ATHARI ZA MRADI NA HATUA ZA UDHIBITI

## MAJI YALIYO CHINI YA ARDHI NA MAJI YALIYO JUU YA ARDHI

### Hali ikoje kwa sasa?

Bomba la mafuta litapita katika mikondo ya maji na ardhi oevu ya bonde la Ziwa Victoria na Tanganyika, bonde la Wami-Ruvu na Pangani pamoja na bonde la kati. Ni sehemu ndogo tu ya mito au mikondo ya maji inayotiririka katika kipindi cha mwaka mzima, mikondo mingine ya maji inakumbwa kiurahisi na mmomonyoko wa udongo. Maji yanayopita juu ya ardhi ni masafi kwa ujumla isipokuwa yanakabiliwa na uchafuzi kutokana na mifugo na shughuli za binadamu. Maji yanayopatikana juu ya ardhi yanatumiwa na binadamu kwa shughuli za kilimo, ufugaji na matumizi ya nyumbani. Maji yaliyo chini ya ardhi ndio chanzo kikuu cha maji kwa jamii ambayo inapitiwa na bomba la mafuta. Uharibifu wa vyanzo vya maji yaliyoko chini ya ardhi kwa kiasi kikubwa unategemea sana uwezo wa udongo na miamba wa kuchuja maji. Kuongezeka kwa idadi ya watu kutasababisha kuongezeka kwa mahitaji ya matumizi ya maji yaliyoko chini ya ardhi.





### Athari zipi zinaweza kutokea?

Maji yaliyoko chini ya ardhi yatatumika katika ujenzi wa kambi na maji yaliyo juu ya ardhi yatatumika katika majaribio ya kupima ubora na uimara wa bomba la mafuta. Utoaji wa maji yaliyo chini ya ardhi unaweza kuleta athari katika mtiririko na ubora wa maji.

### Nini kitafanyika?

Mradi umeanzisha kamati ya upatikanaji wa maji kukabiliana na suala hili. Wizara ya maji na mamlaka husika (ofisi za bonde) zinahusishwa katika mpango huu. Mradi utafanya utafiti wa miamba ya maji ili kuweza kutambua vyanzo muhimu vya maji na pia kuepuka migogoro ya utumiaji wa maji. Hatua za kupunguza athari kama ilivyoelezwa katika mpango wa utunzaji rasilimali, uzuiaji wa uchafuzi, na mpango wa kudhibiti taka zitajumuisha ufuatiliaji wa visima virefu vya maji, uchaguzi wa maeneo ya kutolea maji, na pia mitambo yote ya ujenzi itajazwa mafuta mbali na mikondo ya maji. Mpango wa kudhibiti mmomonyoko wa udongo utaeleza kwa kina hatua za kuzuia na kukabiliana na mmomonyoko wa udongo.

## UDHIBITI WA TAKA

### Hali ikoje sasa?

Wilaya zinazopitiwa na mradi zina uwezo mdogo wa kuchakata taka.





### Athari zipi zinaweza kutokea?

Mradi unaweza kuzalisha aina tofauti za taka ngumu na / taka laini / maji taka ambazo zinaweza kuwa na athari kwa jamii.

### Nini kitafanyika?

Mpango wa kudhibiti taka unauelekeza mradi kupunguza matumizi ya mashimo ya kufukia taka kwa kuzichakata taka, kutumia tena taka katika kutengeneza bidhaa mbalimbali. Mabaki ya chakula yataozeshwa au kuchomwa kwa kutumia mashine maalumu ili kupunguza uhitaji wa kuchimba mashimo ya taka.



# UBORA WA HEWA

## Hali ikoje kwa sasa?

Eneo kubwa la mradi lina hewa nzuri kwa sababu mradi unapita maeneo yasiyo na idadi kubwa ya watu. Uchafuzi wa hewa katika maeneo haya ni mdogo. Hata hivyo kuna kiasi cha vumbi kimegundulika katika baadhi ya maeneo.







### Athari ipi itatokea?

Katika maeneo husika ya mradi ubora au usafi wa hewa unaweza kuathirika na vumbi kutokana na wingi wa magari katika barabara ambazo ni za kiwango cha changarawe na pia kutokana na vifaa vya ujenzi katika mkuza wa bomba.

### Nini kitafanyika?

Upunguzaji wa vumbi utafanyika kwa kuloanisha barabara kwa kutumia maji. Magari na vifaa vyote vitakavyotumika vitatakiwa kuwa katika hali nzuri ili kupunguza uchafuzi wa hewa. Uzalishaji au utoaji wote wa hewa chafu inayotoka katika mitambo utadhibitiwa. Hatua hizi zote zitaelezwa zaidi katika mpango wa kupunguza na kudhibiti uchafuzi wa hewa pamoja na rasilimali za asili.

# KELELE NA MITIKISIKO

## Hali ikoje sasa?

Kwa ujumla sauti zinazosikika katika eneo la mradi ni sauti za shughuli za kilimo, upepo kutokana na mimea, nyimbo za ndege na sauti za magari zinazosikika kwa msimu. Hakuna sauti zozote za viwanda katika maeneo ya mradi.



### Athari ipi itatokea?

Shughuli za ujenzi zinatarajia kuleta mabadiliko ya sauti katika maeneo yaliyo karibu na maeneo ya ujenzi kwa sababu ya shughuli zinazofanywa na magari na mitambo. Kuongezeka kwa idadi ya magari kutachangia kuongezeka kwa sauti kwenye mazingira. Katika ghuba ya Tanga kutakuwa na shughuli za ujenzi zitakazokuwa zinafanyika ndani ya bahari ambazo zinaweza leta athari kwenye mazingira ya bahari.

### Nini kitafanyika?

Kiasi cha sauti kitafuatiliwa na kunakiliwa, pia hatua za pamoja za kupunguza sauti zitatekelezwa.



# AFYA YA JAMII

## Hali ikoje kwa sasa?

Asilimia kubwa ya wakazi katika maeneo ya mradi wanategemea kupata huduma ya afya kupitia vituo vya afya. Matumizi ya dawa za asili yamepungua hasa ukizingatia kwamba watu wengi wanapenda kupata huduma katika vituo vya afya kutokana na kukua kwa maendeleo. Kwa mujibu wa ripoti, kasi ya maambukizi ya Virusi Vya Ukimwi (VVU) imepungua kwa kipindi cha zaidi ya miaka mitano (5) iliyopita kutokana na utoaji wa elimu ya afya, usambazaji na upatikanaji wa mipira ya kujikinga na VVU bila malipo, ongezeko la vituo vya kupimia VVU na upatikanaji wa huduma za matunzo na tiba. Uwezekano wa uwepo wa magonjwa ya mlipuko kama Kipindupindu, Homa ya Matumbo (Typhoid) na Kichocho unabaki kuwa mkubwa katika eneo la mradi kutokana na hali za kiafya, hata kama imeonekana kuna upungufu wa magonjwa ya kuhara.





### Athari zipi zinaweza kutokea?

Kunaweza kuwa na ongezeko la magonjwa ambukizi hasa yale yanayotokana na kujamiiana katika maeneo yatakayopitiwa na barabara zitakazotumiwa na mradi na maeneo ambayo ujenzi wa bomba la mafuta utafanyika. Kuongezeka kwa idadi ya watu katika maeneo ya mradi kunaweza pia kupelekea uhitaji mkubwa wa huduma za afya tofauti na uwezo uliopo.

### Nini kitafanyika?

Kutakuwa na mpango maalum wa kutoa elimu kuhusu hatari za kiafya kwa jamii na wafanyakazi. Mradi utafanya kazi kwa karibu na Serikali za mitaa katika kupunguza hatari za kiafya. Hatua zaidi za kudhibiti na athari zake zitaelezwa kwenye mpango wa afya ya jamii, ulinzi na usalama, ikiwemo upatikanaji wa maji safi, huduma za afya kwa wafanyakazi na kuchimba mitaro kuzuia maji kutuama.

# USALAMA, ULINZI NA USTAWI WA JAMII

## Hali ikoje sasa?

Wanawake, watoto, vijana na makundi ya watu wanao hamahama wana uwezekano mkubwa wa kuweza kupata madhara ya kiusalama, ulinzi na ustawi wa jamii. Uhalifu na unyanyasaji wa kijinsia unaongezeka sana Tanzania, japo kuna jitihada za kupunguza uhalifu zinazofanywa na Serikali na mashirika mengine. Barabara zilizopo mijini na zile zilizopo nje ya mji ni za vumbi, na zinatumika sana na watembea kwa miguu kwa kuwa hakuna sehemu maalum zilizoandaliwa kwa ajili ya watembea kwa miguu. Watumiaji wa baiskeli na boda boda wanazitumia barabara hizi kwa asilimia kubwa hasa katika maeneo ya mijini na uwezekano wa ajali zinazohusu watumia boda boda, watumia baiskeli na watembea kwa miguu ni kubwa zaidi. Msongamano ni nadra sana, isipokuwa katika mpaka na nchi ya Uganda na jijini Dar es Salaam.

### Athari zipi zinaweza kutokea?

Mradi huu unaweza kusabibisha ajali zinazohusiana na kuongezeka kwa idadi ya magari barabarani, hasa wakati wa ujenzi katika maeneo yenye barabara zitakazotumiwa na mradi. Katika maeneo ya ujenzi kutakuwa na hatari ya watu au mifugo kutumbukia katika mitaro iliyowazi na hivyo kusababisha majeraha. Hali ya kutokuwa na usalama inaweza kuongezeka kutokana na ujio wa wafanyakazi na watu ambao wanatafuta ajira.

### Nini kitafanyika?

Utaandaliwa mpango wa kutoa elimu ya juu hatua za ujenzi na changamoto za usalama, ikiwa ni sehemu ya mpango wa afya ya jamii na usalama. Hatua zaidi zitachukuliwa kuhakikisha usalama barabarani ikiwa ni pamoja na kupunguza mwendo kasi na kuajiri madereva ambao wamepitia mafunzo. Vyombo vya usalama vitausaidia mradi na pia vitapatiwa mafunzo juu ya kufanya kazi na jamii. Mradi utahakikisha mitaro inafunikwa kwa wakati. Kutakuwa na alama za usalama, uzio katika maeneo maalum, na pia kutakuwa na mpango wa kutoa elimu ya usalama kwa wafanyakazi na wanajamii.





# MATUMIZI YA ARDHI

## Hali ikoje kwa sasa?

Bomba hili linakatiza katika mikoa 8, wilaya 24, kata 116 na pia linapita karibu vijiji 231 na vitongoji ambavyo vipo pembezoni mwa barabara kuu na barabara ndogo. Shughuli za kijamii za wakazi waliopo katika mradi huu ni za kilimo na ufugaji (kilimo cha mazao na mifugo kutoka sehemu moja hadi nyingine ili kutafuta malisho), pia kuna uchimbaji mdogo mdogo wa madini. Idadi ya wachungaji wa mifugo wanaohamahama imepungua kutokana na sababu mbalimbali zikiwemo kutokuwa na ardhi ya kutosha na pia kuongezeka kwa hifadhi za wanyama. Uchimbaji mdogo wa madini umejikita katika vito vya thamani kama dhahabu na mawe ya thamani (gemstones). Madini mengine yanayochimbwa ni pamoja na chumvi, chokaa, kaolin na jasi (gypsum). Rasilimali za asili zinachangia sana katika sehemu kubwa ya maisha vijijini, zinatumika katika kupikia, kuhakikisha upatikanaji wa chakula, zinatumika kama dawa, chanzo cha mapato na pia zinasaidia katika ujenzi wa makazi.

### Athari zipi zitatokea?







- Kutwaa ardhi ya watu ambayo inatumika kwa kilimo, kuhamishwa kwa watu na makazi na miundombinu mingine.
- Kupungua kwa ardhi ambayo inatumika kwa kilimo, ufugaji, na kupunguza shughuli za kijamii zinazotegemea bahari.
- Migogoro ya ardhi inaweza kuongezeka hasa kwa kuzingatia watu wengi wenye ardhi hawana hati za umiliki.
- Uchimbaji mdogo wa madini unaweza kuathirika katika mikoa ya Tabora, Shinyanga na Geita.

### Nini kitafanyika?

Mradi utatoa fidia kwa watu wenye ardhi, miti, mazao na makazi au miundombinu kutokana na Mpango wa Uhamishaji Watu na Makazi. Kutakuwa na mipango mbalimbali ya kusaidia au kuimarisha maisha ya watu, ikiwa ni pamoja na kupatiwa ardhi ya fidia kwa wale walioathirika. Msaada wa ziada utatolewa kwa watu walio katika hali hatarishi. Mkandarasi atatumia ardhi kwa kuzingatia maeneo mahususi yaliyotengwa na kukubalika kwa kazi.

# HALI YA KIUCHUMI NA KIJAMII

## Hali ikoje kwa sasa?

Biashara za rejareja, kilimo na utoaji wa huduma ndio shughuli kuu katika eneo la mradi. Shughuli za uchumi kwa ujumla ni za kiwango kidogo na nyingi sio rasmi. Wakazi wengi wa pwani wanategemea uvuvi na ukusanyaji wa mabaki ya mazao baada ya mavuno. Pia kuna maeneo maalumu ya biashara kwa wakazi. Idadi ya watu inakua kwa kasi zaidi, hivyo kusababisha uhitaji mkubwa katika huduma za jamii na matumizi makubwa ya rasilimali. Mikoa kama Geita, Tabora na Shinyanga inakabiliana na uhamiaji wa hali ya juu wa watu kutoka katika nchi jirani hususani wakimbizi wanaotokana na migogoro ya kisiasa katika nchi za ukanda wa maziwa makuu.



### Athari zipi zinaweza kutokea?

1. Watu kuacha shughuli zao za kawaida ili kupata ajira katika mradi, hivyo kupunguza uzalishaji katika shughuli za kilimo na kuathirika kwa upatikanaji wa chakula.
2. Uhitaji mkubwa wa bidhaa na huduma wakati wa ujenzi wa bomba la mafuta na hivyo kuathiri upatikanaji wa bidhaa katika eneo la mradi.
3. Kuongezeka kwa watu katika maeneo ya mradi kunaweza kusababisha kutokea kwa ushindani katika upatikanaji wa ajira zilizopo na shughuli nyinginezo za kiuchumi zikiwemo shughuli za biashara.

### Nini kitafanyika?

Kutakuwa na taratibu za wazi na haki katika utoaji wa ajira na kipaumbele cha ajira hususani vibarua na wakazi wa eneo la mradi ili kupunguza ongezeko la watu kutoka maeneo mengine. Mradi utakuwa una ajiri watu wachache na kwa muda mfupi, ili kuwafanya wakazi wa eneo la mradi kutokuacha shughuli zao za kila siku za kiuchumi.

# URITHI WA KIHISTORIA NA KIUTAMADUNI

## Hali ikoje kwa sasa?

Kwa mujibu wa tafsiri ya taasisi za kimataifa, hakuna eneo lolote linalotambuliwa kitaifa na kimataifa kama eneo lenye urithi wa kihistoria katika maeneo ya mradi. Maeneo ya kihistoria yanayohusiana na ufinyanzi, zana za mawe, michoro katika mawe na ushahidi wa kazi za uhunzi yalitambuliwa katika maeneo ya nchi kavu. Urithi wa kihistoria ambao haujatambuliwa unahusishwa na utambuzi wa makundi ya watu au mtu mmoja mmoja; mfano sehemu za matambiko, michezo ya kiutamaduni, ngoma za asili, mila zinazohusisha watu wa kale, dawa za asili, sehemu za mikutano na mito ya kufanyia matambiko, maeneo mengine na vitu vingine muhimu vinaweza tambuliwa baadaye baada ya kushirikisha na kupata taarifa kutoka kwa jamii husika. Upande wa vyanzo vya maji, hakuna maeneo yoyote ya urithi wa kitamaduni yaliyotambulika katika eneo la mradi.







### Athari zipi zinaweza kutokea?

Ukatishaji wa bomba la mafuta katika maeneo yenye urithi wa kihistoria na utamaduni, unaweza kukwamisha maeneo haya ya urithi wa kihistoria na kiutamaduni kufikiwa na watu kwa urahisi. Kunaweza kukawepo na migogoro au migongano ya kiutamaduni kutokana na kuwepo wa tofauti za kiutamaduni, kiimani na kimaadili kati ya wenyeji na wageni. Kunaweza pia kukawa na shida katika kuyafikia maeneo ya kufanyia ibada.

### Nini kitafanyika?

Timu inayofanya kazi na mradi itatambua na kulinda vifaa na vitu vyote vinavyohusiana na urithi wa kihistoria na kiutamaduni wakati wa ujenzi wa bomba la mafuta. Uhamishaji wa maeneo au vituo vya kiutamaduni na makaburi utafanyika kwa kushauriana na viongozi wa eneo husika, jamii na familia husika. Endapo kutahitajika uhamishaji wa makaburi, fidia italipwa kulingana na sheria. Kutakuwa na programu maalumu za kuhamasisha na kujenga uelewa wa wafanyakazi wa mradi juu ya umuhimu wa kuheshimu tamaduni za jamii husika.

# BAYOANUAI

## Hali ikoje kwa sasa?

Sehemu kubwa ya mradi unapita katika maeneo ambayo yamebadilishwa na binadamu. Maeneo ya kilimo na mifugo hayana nafasi kubwa kwa bayoanuai. Baadhi ya maeneo ni makazi ya asili na baadhi ya maeneo haya yanalindwa kisheria na ni maeneo ya kipekee nchini Tanzania. Kuna makazi ya asili ambayo yanaweza kubadilika kwa haraka na yako katika hali hatarishi. Asilimia kubwa ya maeneo haya yamekwepwa katika upitishaji wa bomba la mafuta. Eneo ambalo litatumika kama kituo cha kufunika mabomba ili yaweze kutunza joto kwa ujumla linatumika kwa kilimo. Hata hivyo eneo hili lipo ndani ya ukanda wa kati na mashariki wa misitu ya miombo ambayo inapita katika nchi kumi zilizopo Afrika ya kati na kusini. Rasi ya Chongoleani inajumuishwa katika Msitu wa Pwani ya Afrika Mashariki ambayo ni muhimu kwa makazi na uhifadhi wa ndege na sehemu muhimu ya bayoanuai. Usafishaji makazi ya asili kwa ajili ya malisho ya mifugo, kilimo, uchomaji moto na upasuaji wa mbao ndio vihatarishi vikubwa kwa misitu iliyopo pwani, na hali hii inaoneka kwamba itazidi kuongezeka. Eneo kubwa ambalo tanki la kuhifadhi mafuta litajengwa limeshaathirika kutokana shughuli za kilimo na kwa hiyo limetengwa kama eneo la asili kwa kiasi fulani.





### Athari zipi zitatokea?

Wanyama pori na mimea inaweza kuathirika kwa sauti na mitikisiko; wanyama wa nchi kavu na viumbe wa majini wanaweza kuathirika na shughuli za mradi. Zaidi ya hapo, utwaaji wa ardhi kwa matumizi ya mradi unaweza pia kuleta athari katika bayoanuai.

### Nini kitafanyika?

Hatua za mradi zinazolenga kuepuka kuathirika na kutoweka kwa bayoanuai zitaandaliwa na kutekelezwa. Hatua hizi zitajumuisha elimu kwa wafanyakazi na jamii, pamoja na elimu juu ya uhifadhi wa bayoanuai na mipango ya kupunguza athari za mradi na kuleta tija kwa bayoanuai zitatolewa.

# MAZINGIRA YA BAHARINI



## Hali ikoje sasa?

Pwani ya Tanga ina utajiri wa bayoanuai na thamani ya uhifadhi. Mkoa wa Tanga una idadi kubwa ya maeneo yanayotambulika kiekolojia na kibaiolojia kitaifa na kimataifa ikiwa ni pamoja na Hifadhi ya Bahari ya Silikanti Tanga (TCMP), Hifadhi ya Bahari ya Ulenge na Kwale, Tanga North-Kibo Saltpans na idadi kubwa ya miradi ya kijamii inayolenga kudhibiti maeneo ya pwani. Maeneo makubwa ya pwani ya Tanga yanakabiliwa na uharibifu wa mazingira kutokana na ongezeko la kukua kwa mji na shughuli za kijamii. Shughuli za uvuvi haribifu na usio endelevu, ukataji wa miti na shughuli za kilimo ambazo zinasababisha kutuama au kuongezeka kwa udongo/mchanga na uchafuzi mwingine ambao unaathiri mazingira ya bahari. Hivi vyote vina athari kwenye rasilimali za baharini, ambazo watu na mazingira wanavitegemea. Asilimia kubwa ya wakazi wa Tanga wanategemea uvuvi zaidi kwa maisha yao zaidi ya kilimo.



### Athari zipi zitatokea?

Mradi huu unaweza kusababisha athari za kimazingira na pia unaweza kuwaathiri baadhi ya viumbe wa ardhini na baharini (ikiwa ni pamoja na uwezekano wa kuathiri wanyamapori, mamalia wa bahari kama nyangumi na pomboo, kasa, ndege na samaki pamoja na mazalia yao kama vile matumbawe, mikoko na majani ya baharini).



### Nini kitafanyika?

Mradi utadhibiti athari kwenye mazingira ya bahari wakati wa ujenzi wa bomba la mafuta na baada ya ujenzi. Hatua hizi ni pamoja na kutumia mbinu zitakazo punguza sauti na mitikisiko, na mbinu ambazo zitazuia utengenezaji wa vumbi na tope wakati wa ujenzi. Kutakuwa na uangalizi wa mamalia baharini na iwapo pomboo au nyangumi wataonekana katika mazingira basi shughuli za ujenzi zitasimama kwa muda hadi watakapoondoka katika eneo husika. Katika kudhibiti athari za mazingira zitokanazo na kuvuja kwa mafuta, mradi utashirikiana na Serikali ya Tanzania ili kuingiza mradi katika mpango wa kuthibiti umwagikaji wa mafuta (National Oil Spill Contingency Plan). Mradi utatumia mbinu za ziada za uhifadhi ili kudhibiti mazingira ya bahari and kulinda bayoanuai ya ghuba ya Tanga.



**MRADI WA EACOP - TANZANIA**
Total EAST Africa Midstream B.V,
Msasani Peninsula, 429 Barabara ya Mahando, Kitalu D,
S.L.P 38568, Dar es Salaam, Tanzania.
Simu: +255 22 2214100 / 4102/4103
Barua Pepe: EACOP.info@total.com
www.eacop.com

**MRADI WA EACOP - UGANDA**
TEAM - Total East Africa Midstream
Kiwanja Namba 21, Barabara ya Yusuf Lule,
S.L.P 34867, Kampala - Uganda
Simu: 0800 216 000 (Isiyo na Makato) au +255 (0) 204 916 000
Barua Pepe: EACOP.info@total.com
www.eacop.com

© 2020. Haki zote zimehifadhiwa.
Kijarida hiki au sehemu yoyote ya kijarida hiki hairuhusiwi kuchapishwa, kuhaririwa, kuhifadhiwa au kusambazwa kwa namna yoyote ile bila ya kuwa na idhini ya maandishi ya Utawala wa Bomba la Mafuta Ghafi - Afrika Mashariki.